

MIKUTANO YA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Kanuni ya 28 ya Kanuni za Kudumu za Bunge inatoa utaratibu wa Bunge kukutana kwa ajili ya Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya kama ifuatavyo: -

(1) Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya utafanyika mahali, tarehe na saa ambayo Rais atamka kupitia tangazo litakalochapishwa katika Gazeti wakati akiitisha Mkutano wa Bunge Jipya.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni hizi kuhusu kuanza, kusitishwa au kuahirishwa kwa vikao vya Bunge, Mkutano wa Kwanza wa Bunge utaendelea kwa muda wowote ambao utahitajika kwa ajili ya kutekeleza na kukamilisha Shughuli zote za Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya.

Kanuni ya 33 ya Kanuni za Kudumu za Bunge inatoa utaratibu wa Bunge kukutana katika Mikutano ya Kawaida ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ifuatavyo: -

(1) Isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo, kila Mkutano wa Bunge utafanyika katika Ukumbi wa Bunge Dodoma.

(2) Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zitapigwa na kuimbwa katika kila kikao cha kwanza na cha mwisho kwa Mikutano yote ya Bunge kufuatana na utaratibu utakaowekwa na Bunge.

(3) Bila ya kuathiri masharti yanayofuata ya Kanuni hii, kila Mkutano isipokuwa Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya, utaanza tarehe itakayotajwa na Bunge.

(4) Endapo manufaa ya Taifa yatahitaji kuwa Bunge lisikutane tarehe ile iliyowekwa kwa Mkutano utakaofuata, bali likutane tarehe ya mbele zaidi au ya nyuma zaidi, basi Spika anaweza, kuliita Bunge likutane tarehe hiyo ya mbele zaidi au nyuma zaidi.

(5) Iwapo Bunge litatakiwa kukutana tarehe ya mbele zaidi kuliko tarehe za iliyotangazwa awali, basi tarehe hiyo mpya haitakuwa mbele zaidi ya siku kumi na nne kutoka tarehe iliyotangazwa hapo awali.